Hati ya kweli 2 ya Rejista ya Walezi

Taarifa kwa ajili ya walezi na wanachama wa kaya: Ni data gani zinarekodiwa?

Oktoba 2015

Kuhusu Ofisi ya Mlezi wa Mtoto (OCG) ya NSW

OCG ni mamlaka huru ya kisheria yenye nia ya kuhakikisha matokeo bora kwa watoto na vijana wakikwepo katika utunzaji nje ya makazi (OOHC) uliosaidiwa na serikali. OCG ni mdhibiti – siyo mtoaji wa huduma za utunzaji.

OCG hudhibiti na kufuatilia utendaji wa mashirika yanayopanga utunzaji nje ya makazi (OOHC) na huduma za kitendo cha kupanga mtoto zinazosaidiwa na serikali. OCG inasimamia Rejista ya Walezi, kifadhio cha data ya watu wenye mamlaka au wakiomba kutoa utunzaji nje ya makazi (OOHC) uliosaidiwa au ya serikali huko NSW. Wanachama wa kaya pia wanarekodiwa kwenye hiki kifadhio cha data.

OCG husajili na kufuatilia mashirika yanayotoa, kupanga au kusimamia utunzaji wa hiari nje ya makazi (OOHC).

Rejista ya Walezi

Rejista ya Walezi ni mfumo salama wenye vikwazo vya kupatikana. Mfumo huu uliobuni ili kuimarisha mchakato wa kutoa mamlaka na kusaidia ushirikiano bora wa taarifa kati ya mashirika husika.

Haichukui nafasi ya mifumo na michakato pana yanayotumia mashirika kutathmini waombaji kuwa mlezi na wanachama wao wa kaya, na kutoa mamlaka kwa watu binafsi wanaofaa kuwa walezi wenye mamlaka.

Rejista ya Walezi inarekodi taarifa za nani?

Rejista ya Walezi inahifadhi taarifa kuhusu:

- waombaji kuwa mlezi (watu binafsi wanaotoa ombi kwa shirika husika ili wawe walezi wenye mamlaka)
- walezi wenye mamlaka (watu binafsi walioidhinishwa na shirika husika kutoa utunzaji nje ya makazi (OOHC) uliosaidiwa au ya serikali, ikijumuisha wale wenye mamlaka mbili kuwa walezi na wazazi wa kupanga)
- wanachama wa kaya (watu wazima, vijana na watoto wakiishi kama kawaida kwenye nyumba ya mlezi au kukaa kwenye makazi yalioyounganishwa na ile nyumba, kwa mfano fleti ndogo au msafara).

Watoto na vijana wakikwepo kwenye utunzaji nje ya makazi (OOHC), uliosaidiwa au wa hiari, **hawata**rikordiwa kwenye Rejista ya Walezi. Hata hivyo, kama wataendelea kuishi kwenye nyumba ya mlezi baada ya kutimiza umri wa miaka 18, wanapaswa kurekodiwa kwenye Rejista ya Walezi na wawe na Ukaguzi wa Kufanya Kazi na Watoto wa NSW ya kisasa.

Locked Bag 5100
Strawberry Hills, NSW 2012
Simu: 02 8219 3600
Faksi: 02 8219 3699
ABN 43 304 920 597c
carers-register@kidsguardian.nsw.gov.au
www.kidsguardian.nsw.gov.au

Rejista ya Walezi inahifadhi taarifa gani?

Rejista ya Walezi hurekodi taarifa za kitambulisho kuhusu waombaji kuwa mlezi na walezi wenye mamlaka, na wanachama wao wa kaya ikijumuisha majina yao, majina ya zamani, jinsia, na kama wanajitambua kuwa Mtu wa Asili au Mwenyeji wa Kisiwa cha Torres Strait.

Taarifa kuhusu kaya zinazorekodiwa zinajumuisha anwani ya makazi, orodha ya watu wote wanaoishi nyumbani na matokeo ya ukaguzi wa nyumba. Mahusiano kati ya walezi na wanachama wa kaya yanarekodiwa, ikijumuisha shughuli za kuingia na kutoka kwenye kaya za walezi.

Walezi na wanachama wa kaya vilevile wanaulizwa kama wana mahusiano yoyote na shirika lingine husika lolote huko NSW au kwenye jimbo au kanda lingine lolote la Australia.

Ombi la mlezi na kumbukumbu yake ya mamlaka, ikijumuisha kukataliwa maombi na ufutaji wowote au uahirishaji wa mamlaka unarekodiwa kwenye Rejista ya Walezi.

Kupata taarifa zaidi, rejelea Hati ya Kweli 1 ya Rejista ya Walezi: Kukagua uaminifu na ustahiki wa walezi na wanachama wa kaya.

Matokeo ya ukaguzi ya sharti ya uaminifu na ustahiki

Rejista ya Walezi inarekodi matokeo ya kukagua na kutathmini mwombaji kuwa mlezi na mwanachama wa kaya na hairuhusu mlezi kupewa mamlaka yote mpaka shirika husika linathibitisha na kukidhi kikamilifu ukaguzi na tathmini zote zinazotakiwa.

Rejista ya Walezi haihifadhi kila kitu kuhusu kila ukaguzi wa uaminifu na ustahiki, ni matokeo tu (kwa mfano matokeo ya kuridhisha au kutoridhisha).

Hata hivyo, mashirika husika yanatunza kumbukumbu za maelezo yote na hiyo yanaweza kushirikiana na mashirika mengine husika wakati wa ‘ukaguzi mwingine wa shirika husika’.

Shirika husika linapaswa kuwasiliana na mashirika mengine husika kuhusu mwombaji kuwa mlezi au mwanachama wa kaya ambaye inajulikana kwamba ana mahusiano ya kisasa au ya zamani na shirika lingine husika. Nia ya ukaguzi huu ni kuhakikisha kwamba taarifa zinazohusu tathmini ya waombaji kuwa mlezi inashirikiana na mashirika husika.

Taarifa ya dai inayoripotiwa

Rejista ya Walezi huonyesha wakati shirika linachunguza dai inayorepotiwa au

wakati ofisi ya Mchunguzi Maalum inatoa maelekezo kwa hilo shirika kwamba dai haitakiwi kukamilishwa kwenye Rejista. Kwa kuongeza, rekodi ya kudumu ya madai yanayoripotiwa inatunzwa wakati shirika husika linaamua kwamba kunaweza kuwa na hatari zinazoendana na usalama, ustawi au uhai wa mtoto katika utunzaji nje ya makazi (OOHC).

Rejista ya Walezi hurekodi tarehe na hali ya tarehe ya dai, lakini hairekodi maelezo ya dai. Taarifa kuhusu madai kamili yanayoripotiwa (na baadhi ya madai ya kisasa yanayoripotiwa), yanaweza kushirikiana na mashirika mengine kama sehemu ya 'ukaguzi wa shirika lingine husika'.

Kurekodi taarifa ya mlezi na mwombaji kuwa mlezi

Mashirika husika yanapaswa kutoa taarifa kwa walezi wenye mamlaka na wanachama wao wa kaya; na ili kufuata sheria, taarifa za waombaji kuwa mlezi na wanachama wao wa kaya zinapaswa kuandikwa kwenye Rejista ya Walezi.

Si lazima kupata ruhusa kutoka kwa walezi wenye mamlaka na wanachama wao wa kaya ili taarifa zao ziandikwe kwenye Rejista ya Walezi, lakini mashirika husika yanapaswa kuwatolea taarifa kuhusu taarifa gani zitakazorekodiwa.

Waombaji kuwa mlezi na wanachama wa kaya hawalazimishwi kutoa ruhusa lakini bila hiyo ombi lao kupewa mamlaka haliwezikani kuendelea.

Nani anaweza kupatikana taarifa za Rejista ya Walezi?

Shirika husika pekee linaweza kupatikana taarifa ya Rejista ya Walezi kuhusu walezi wao na wanachama wa kaya, lakini wanaweza kupatikana kumbukumbu yoyote kwenye Rejista ya Walezi ya mtu binafsi anaejaza ombi kwa mashirika kupata mamlaka kama mlezi au anaanza kuwa mwanachama wa kaya (wa mwombaji kuwa mlezi au mlezi mwenye mamlaka).

OCG, Idara ya Huduma za Familia na Jamii (Department of Family and Community Services) na Mchunguzi Maalum huko NSW wanaweza kupatikana taarifa za Rejista ya Walezi. Wanaotekeleza sheria, baraza za uchunguzi na kulinda watoto katika mamlaka nyingine zinaweza kupewa taarifa zinazohifadhiwa kwenye Rejista ya Walezi.

Waombaji kuwa mlezi, walezi wenye mamlaka na walezi wa zamani, na wanachama wao wa kaya wanaweza kupatikana taarifa kuhusu wao wenyewe zilizohifadhiwa kwenye Rejista ya Walezi ikijumuisha taarifa kuhusu watoto wao. Ni sharti kushauriana na Mchunguzi Maalum kabla ya kufichua taarifa zinazohusu uchunguzi kutokukamilika na kuelekea madai yasiyoripotiwa na baadhi ya maswala kuhusu tabia inayoripotiwa.

Nani anaingiza na kusasisha taarifa kwenye Rejista ya Walezi?

Shirika husika linalotoa mamlaka kwa mlezi linawajibu wa kuingiza taarifa kuhusu ombi la mlezi na kutoa mamlaka kwenye Rejista ya Walezi. OCG itatunza Rejista ya Walezi kulingana na *Children and Young Persons (Care and Protection) Act 1998* na *Children and Young Persons (Care and Protection) Regulation 2012.*

Taarifa Zaidi

Taarifa kuhusu Rejista ya Walezi inapatikana kwenye tovuti ya OCG kwa: www.kidsguardian.nsw.gov.au. Kama una maswali yoyote, tafadhali tuma barua pepe kwa walezi-register@kidsguardian.nsw.gov.au.

Kupata taarifa kuhusu wajibu wengine wa kisheria wa OCG, ikijumuisha Ukaguzi wa Kufanya Kazi na Watoto, Taasisi za Mtoto Salama, Utunzaji Huru na ya Sheria Nje ya Nyumba, na Kitendo cha Kupanga Mtoto, tafadhali tembelea www.kidsguardian.nsw.gov.au.

Hati ya Kukataa: Taarifa inayotumia kwenye hati hii ya kweli ni mwongozo tu. Kila jitihada ilitumika kuhakikisha kwamba taarifa yote ni sahihi, ya kisasa na ya kweli. Hata hivyo, hatuwezi kuhakikisha hiyo daima na hakuna kudhamini kwamba taarifa ni bila kosa wala kitendo cha kuacha. Watumizi wanapaswa kuwa waangalifu na kutumia ujuzi wao kulingana na matumizi ya taarifa. Pia taarifa hizo haziwezi kuchukua nafasi ya ushauri huru ya kisheria au ushauri mwingine kutoka kwa mtaalam na watumizi wanatakiwa kupata ushauri kutoka kwa mtaalamu unaofaa na kuendana na hali yao mahsusi.

Ofisi ya Mlezi wa Mtoto haidhamini, wala kukubali wajibu wowote wa kisheria juu ya kitendo chochote kilichofanyika, kitendo cha kuacha, kupoteza, kuharibu, gharama wala usumbufu kutokana na, kuhusiana na, au kama matokeo ya, kutumia au kutegemea taarifa zinazopatikana kwenye hati hii ya kweli.

www.kidsguardian.nsw.gov.au
Oktoba 2015